

Maktaba ya Jiji – Mfumo wa Maktaba za Umma Salt Lake City
Nambari hii ya Kadi ya Maktaba inaweza kutumia kuanzia Septemba 1.

Itunze kwa kumbukumbu zako – usiiache shuleni

Jina la Mwanafunzi:

Nambari ya Muda ya Kadi ya Maktaba

Nambari ya PIN ya Mwanafunzi yenye Tarakimu 4
(unaweza kuipata ofisini)

Nambari hii ya muda ya Kadi ya Maktaba na nambari ya PIN yenye tarakimu 4 itamuwezesha mtoto wako kupata rasilimali za maktaba; ikiwemo kuingia kwenye kompyuta, taarifa za akaunti kwenye hifadhi data, na kutuma maombi. Nambari hii ya PIN kimsingi ni tarakimu 4 za mwisho za nambari ya simu iliyoandikwa kwenye nyaraka za mtoto husika za usajili shuleni. Kama hakuna nambari ya simu iliyoandikwa, nambari ya PIN yoyote ile yenye tarakimu 4 itatengenezwa. Wazazi hawataweza kuibadilisha nambari ya PIN hapo mwanzoni, lakini inaweza kubadilishwa itakapofikia tarehe ya hapo baadae kwa kuingia kwenye akaunti ya kadi ya maktaba ya mtoto husika kupitia [www. Slcpl.org](http://www.Slcpl.org). Itunze vizuri nambari hii ya PIN na hakikisha mtoto wako anaikariri.

Ingawa Kadi hii ya muda ya Maktaba haina ukomo wa matumizi, unaweza kufikiria kuiboresha akaunti ya Maktaba ya mtoto wako kuwa Basic Card. Basic Card inaongeza ule ukomo wa mtoto wako wa kuchukua vifaa hadi kufikia 13, kwa ukomo wa CD 3 na DVD 3.

Ili kupata kadi halisi au kuiboresha akaunti ya mtoto wako kuwa Basic Card, utahitajika kuleta nambari yake ya muda ya Kadi ya Maktaba kwenye Maktaba yoyote ya Jiji sambamba na taarifa zifuatazo za anwani ya sasa ya makazi ya mzazi wa mtoto au mlezi halali kisheria.

- ID rasmi yenye picha na jina, taraha ya kuzaliwa, na anwani ya sasa
- Nyaraka rasmi na ya hivi karibuni inayotumwa kwa njia ya posta, kama vile bili ya umeme au maji au kadi ya mkopo, inaweza kutumika sambamba na ID yenye picha ili kuonesha anwani sahihi ya makazi.

Kwa kawaida, wakazi wa nje ya Salt Lake County wanahitajika kununua kadi ya Maktaba ya Jiji kwa \$80 kwa mwaka. Hata hivyo, mtoto yeyote mdogo kwa mujibu wa sheria anayesoma katika Wilaya ya Shule za Salt Lake City, bila kujali kata ya makazi anafuzu kupata kadi ya bure ya Maktaba ya Jiji, hivyo anasamehewa ada hii.

Saini ya Mzazi:

Tarehe ya kusainiwa: